



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA
WATOTO

BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA

Tovuti: www.hlpc.go.tz



TANGAZO

KUJIUNGA KWENYE MFUMO WA MAFUNZO YA MASAFI MAREFU

KWA NJIA YA MTANDAO (National eLearning Platform for Health)

Baraza la Wataalamu wa Maabara linachukua nafasi hii kuwajulisha Wataalamu wote kuwa Wataalamu wote wenye usajili wa kudumu (FRP & ERP) wanatakiwa kulipia ada za mwaka kila mwaka wa fedha wa Serikali. Sambamba na hilo Wataalamu wote wenye usajili wa kudumu wanatakiwa kujiendeleza kwa kuhudhuria mafunzo endelevu (CPD Courses) ili kuendelea kuboresha taaluma zao na utaalamu kazini.

Baraza la Wataalamu wa Maabara limefanikiwa kuunganisha mfumo wa usajili wa Wataalamu (HPRS) na mfumo wa mafunzo kwa njia ya masafu marefu (National eLearning Platform for Health) ili kuwawezesha Wataalamu wake wenye usajili wa kudumu kuweza kuhudhuria kozi zinazotolewa.

Wataalamu ambao tayari wana akaunti kwenye mfumo wa usajili wa HPRS (hprs.moh.go.tz) watatumia akaunti zao (Email na Password) kuweza kuingia kwenye mfumo wa mafunzo kwa masafu marefu (<http://elearning.moh.go.tz>).

Hatua orodheshwa zitafuatwa kwa mtaalam atakapotembelea mfumo wa mafunzo ya masafu marefu kwa njia ya mtandao:

- I. Bofya **CPD Courses**, [click here](#)
- II. Username tumia Email uliyosajiliwa kwenye mfumo wa HPRS
- III. Password: Rudia kujaza Email uliyosajiliwa kwenye wa HPRS

Utafanikiwa kuingia na utatakiwa kubadilisha nywila (Password)

- IV. Current Password: jaza Email yako
- V. New Password: Jaza Password unayotumia kwenye mfumo wa HPRS
- VI. New Password (Again); Rudia kujaza Password unayotumia kwenye mfumo wa HPRS kisha save changes.

Mtaalam atakapomaliza kozi na kukidhi vigezo elekezi atapatiwa cheti cha kozi husika na atakusanya pointi za CPD ambazo zitaonekana kwenye akaunti yake ya mfumo wa Usajili (HPRS)

Ofisi ya Msajili inawasisitiza wataalam wote ambao wanausajili wa kudumu kuhakikisha wanasajiliwa kwenye mfumo wa HPRS na Wataalam wote wenye usajili wa kudumu ambao wameshasajiliwa kwenye mfumo wa HPRS kujisajili kwenye mfumo wa mafunzo ya masafa marefu kwa njia ya mtandao.

Mawasiliano Simu: 0734005777, Email: hlpc@afya.go.tz

Imetolewa na:



Msajili

Baraza la Wataalam wa Maabara

